



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA KILIMO
TUME YA MAENDELEO YA USHIRIKA TANZANIA



TANGAZO KWA UMMA

MAONI YA MABORESHO YA KANUNI ZA VYAMA VYA USHIRIKA ZA MWAKA 2015

Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC) ipo katika hatua ya maboresho ya Kanuni za Vyama vya Ushirika za Mwaka 2015, kwa lengo la kuimarisha udhibiti na uhamasishaji wa Vyama vya Ushirika nchini.

Kwa kutambua mchango wa wanaushirika na wadau wake katika kukuza na kuboresha Sekta ya Ushirika nchini, TCDC inawaalika Wanaushirika na Wadau wa Sekta ya Ushirika kuwasilisha maoni kwenye maeneo ambayo wanaona yanahitaji kufanyiwa maboresho/marekebicho kwenye Kanuni za Vyama vya Ushirika za Mwaka 2015.

Maoni hayo yawasilishwe kwa maandishi kupitia barua pepe: ushirika@ushirika.go.tz, kabla/ ifikapo tarehe 31/12/2024 ili kuwezesha taratibu nyingine ziweze kuendelea.

Kwa maulizo na ufafanuzi zaidi wasiliana na Albert Mwombeki, kupitia simu ya mkononi namba 0688 40 5748 au email: albert.patrick@ushirika.go.tz au Lilian Lyimo, simu ya mkononi namba 0714 973628 au email: lilian.lyimo@ushirika.go.tz

Imetolewa na:

KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI,
TUME YA MAENDELEO YA USHIRIKA TANZANIA

05/12/2024